

Ijaribu na **Uikarabati**

Marudio ya KCSE

KISWAHILI

Toleo jipya

OXFORD

Utangulizi

Ijaribu na Uikarabati ni kimoja kati ya msururu wa vitabu vya marudio vya **Test it & fix it**. Kitabu hiki kitakusaidia kufikia uwezo wako wa kupata alama za juu katika mtihani.

Tofauti na vitabu vingine vya marudio, kitabu hiki kinakupa videokezo vya kukusaidia kujibu maswali kwa kukueleza kile ambacho watahini hutarajia kutoka kwa watahiniwa. Kitabu hiki kimeandikwa na kuhaririwa na watahini walio na tajiriba kubwa katika utahini wa mtihani wa KCSE.

Ijaribu na Uikarabati, Marudio ya KCSE kimeshughulikia mada zote zinazotahiniwa katika karatasi zote tatu za lugha ya Kiswahili.

Sehemu ya kwanza inashughulikia **yaliyomo kwenye silabasi** ya Kiswahili kwa shule za upili.

Sarufi na matumizi ya lugha ndiyo inayotangulia ikifuatwa na ufahamu na ufupisho, kisha isimujamii. Mada hizi zinajumuisha yaliyomo kwenye silabasi kuhusiana na karatasi ya mtihani wa Sarufi na matumizi ya lugha.

Yaliyomo kwenye silabasi kuhusiana na karatasi ya insha na utungaji yanafuata. Haya ni pamoja na tungo zote za kiamilifu, tungo za kitaaluma na insha za kubuni.

Sehemu ya kwanza inatamatishwa na karatasi ya tatu ambayo ni Fasihi. Karatasi hii hujumuisha ushairi, vitabu viteule na fasihi simulizi.

Sehemu ya pili inajumuisha maswali ya **mwigo wa mitihani** kwa karatasi zote tatu.

Sehemu ya mwisho ina **majibu** ya maswali yote kwenye kitabu hiki, ikiwa ni pamoja na majibu ya maswali yote ya mwigo wa KCSE.

Mada kuu katika sehemu ya kwanza zinaanza kwa shabaha ambazo mwanafunzi anatarajiwa kuafikia katika kila sehemu. Shabaha hizi zitamwongoza mwanafunzi kujuua matarajio ambayo atatahiniwa kwayo. Aidha, katika kitabu kizima kuna vipengele viliviyotumika kukusaidia kufikia upeo wa uwezo wako katika mtihani. Vipengele hivi ni kama ifuatavyo:

Shabaha:

Huu ni muhtasari wa yale ambayo mwanafunzi anatarajiwa kuweza kutimiza kufikia mwisho wa kila sehemu. Unashauriwa kujihakiki iwapo umeweza kuyaafikia.

Marejeleo: Yanakueleza pale ambapo unaweza kurejelea maelezo zaidi kuhusiana na swali la mada.

Tahadhari

Haya ni baadhi ya makosa ambayo wanafunzi hufanya mara kwa mara. Yapo mapendekezo ya jinsi ya kuyaepuka.

Siri ya Kufaulu

Hivi ni videokezo vya kukuwezesha kujuua kile ambacho mtahini anatarajia katika majibu na jinsi ya kufikia matarajio hayo.

Zoezi

Haya ni maswali ya kufanya mazoezi dhana ambayo imefundishwa.

Mifano

Hii ni mifano iliyotolewa ili kukuonesha jinsi ya kujibu maswali.

Zoezi la ziada

Zaidi ya maswali ya zoezi baada ya kila mada, hili ni zoezi la kuongezea baada ya mada kadha. Mwanafunzi anashauriwa kulifanya ili kujinua kistadi.

Kumbuka

Hivi ni videokezo muhimu vya kukumbuka ili uweze kufikia upeo wa ufanisi.